

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA MOROGORO



Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. MDC/E.70/5/19

Tarehe: 13 Aprili, 2021.

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Halmashauri ya Wilaya Morogoro imepokea Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na. **FA.170/361/01”A”/92** cha tarehe **17 Machi, 2021** kutoka kwa Katibu Mkuu (Utumishi). Kufuatia kibali hicho, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya Morogoro anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa za kujaza nafasi nne (04) za kazi ya Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II.

**1.0 NAFASI: MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (NAFASI 04)**

**1.0.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na Wasomaji,
- ii. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka na utoaji wa nyaraka,
- iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka au nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (classification and boxing) kwaajili ya matumizi ya ofisi,
- iv. Kuweka/kupanga kumbukumbu na nyaraka mbalimbali kwenye mafaili,
- v. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (file racks/cabinets) katika masijala/vyumba vya kuhifadhia Kumbukumbu.
- vi. Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka) katika mafaili
- vii. Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Taasisi za serikali.
- viii. Kufanya kazi nyingine kama atakavyopangiwa na kiongozi wake zinazohusiana na elimu na ujuzi wake wa kazi.

**1.0.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Awe amehitimu Kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form VI)
- ii. Awe na Cheti cha Utunzaji Kumbukumbu (NTA Level 5) katika mojawapo ya fani za afya, masijala, mahakama na ardhi.

**1.0.3 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia muundo na ngazi za mishahara ya Watumishi wa Serikali yaani **TGS B** kwa mwezi.

#### 1.0.4 MAMBO YA JUMLA YA KUZINGATIA

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania
- ii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- iii. Nafasi hizi zitajazwa kwa masharti ya mkataba kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hivyo mwombaji awe tayari kupangiwa na kufanya kazi katika Kituo cha kazi chochote ndani ya Halmashauri kulingana na mahitaji ya kazi.
- iv. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma walioajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni hawatakiwi kuomba nafasi hizi.
- v. Waombaji waambatishe Maelezo Binafsi yanayojitoshleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
- vii. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and Form VI Results Slips) HAVITAKUBALIWA.
- viii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- x. Waombaji kazi ambao tayari ni Waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi, Wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Aprili, 2021.**

Maombi yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya Morogoro,  
S.L.P. 1880,  
**MOROGORO.**

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ambayo ni [www.morogorodc.go.tz](http://www.morogorodc.go.tz), tovuti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ambayo ni [www.ajira.go.tz](http://www.ajira.go.tz) pamoja na mbao za matangazo za Halmashauri.

Imetolewa na:-

Rehema S. Bwasi

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**

STRICT EXECUTIVE DIRECTOR  
MOROGORO DISTRICT COUNCIL